

MWONGOZO WA 102/1 BUNAMFAN-JUNI 2022

1. Wewe ni chifu wa kata ya Mwangaza. Umeandaa mkutano wa wanakata wako. Andika hotuba utakayotoa kuhusu mambo yanayoathiri utangamano wa kitaifa na hatua zinazoweza kuchukuliwa.

JIBU

-Hii ni insha ya kiuamilifu

-kichwa kionyeshe; mada na hadhira lengwa

Neno hotuba sharti liwepo

-UTANGULIZI

- a) Huanza kwa kutaja watu kwa vyeo vyao na majina yao rasmi.
- b) Aliye na cheo cha juu zaidi hutambuliwa kwanza ukielekea chini/itifaki izingatiwe.
- c) Hufuatiwa na maamkuzi
- d) Baadaye lengo la hotuba yenyewe.

MWILI

- a) Ndicho kiina cha hotuba
- b) Huanza katika aya ya pili
- c) Kila hoja hufafanuliwa katika aya yake.
- d) Ili hoja ya mtahiniwa ikamilike lazima mwanafunzi azingatie hatua zifuatazo:
Ataje hoja, aieleze na ataje hatua zinazoweza kuchukuliwa kusuluhisha mambo yanayoathiri utangamano wa taifa (katika aya moja).

HOJA

MAMBO YANAYOATHIRI UTANGAMANO WA KITAIFA

- a) Ufisadi kama vile kuajiri watu kwa mapendeleo
- b) Ukabila
- c) Viongozi kueneza chuki/uchochezi
- d) Mafunzo hasi ya kidini/
- e) Ukosefu wa ajira/utabaka
- f) Kubagua maeneo Fulani kimaendeleo.
- g) Ukimbizi wa ndani kwa ndani
- h) Mashambulizi ya kigaidi/kikoo/kijamii

- i) Migogoro ya ardhi/mipaka ya kijamii

Hatua zinazofaa kuchukuliwa

- a) Lugha ya taifa kuhimizwa
- b) Kukabiliana na ufiadini
- c) Usawa katika ugawaji wa raslimali
- d) Kuelimisha kuhusu umoja wa kitaifa/hamasisho
- e) Tamasha za kitamaduni
- f) Kutalii sehemu zingine za nchi
- g) Ndoa za makabila tofauti/ndoa za mseto
- h) Serikali ya muungano
- i) Viongozi wachochezi kuchukuliwa hatua kisheria

HITIMISHO

Hatibu kuwashukuru wote waliohudhuria kwa muda wao na utulivu wao wakati wa kumsikiliza.

TANBIHI

- a) Alama za mtajo hazitumiki
- b) Hoja zisipungue nane

visit www.freekcepastpapers.com to download free resources

2. Fafanua hatua ambazo zimechukuliwa nchini ili kukabiliana na tatizo la unyanyasaji wa jinsia ya kike.

HOJA

- a) Hatua kali za kisheria kwa wanaowapiga na kuwabaka, na wanaotekeleza mila ya kuketa na ndoa za mapema
- b) Kufanya kampeni dhidi ya mila zinazochangia udunishaji wa wanawake
- c) Kuwashauri watoto wa kike waende shuleni
- d) Kuanzisha makao ya watoto wa kike wanaotishiwa na mila mbaya
- e) Kuelimisha mwanamke kuhusu haki zake
- f) Kuhimiza wanawake kupigania haki zao
- g) Serikali kutenga pesa za kuelimisha watoto wa kike
- h) Kuwepo kwa mashirika ya kutetea haki za wanawake kama FIDA na maendeleo ya wanawake.
- i) Hazina ya kutoa mikopo kwa wanawake kama K.W.F.T
- j) Kuwapa wanawake nafasi sawa za ajira
- k) Kutekelezwa kwa kipengele cha thuluthi mbili ya wanawake katika uongozi
- l) Kupunguza alama ambazo wasichana wanapaswa kufikisha ili kujiunga na vyuo vya elimu ya juu
- m) Kubuni sheria za kuwawezesha kumiliki mali

TANBIHI

-Kadiria hoja za mwanafunzi

-Ili hoja iwe kamili, mtahiniwa ataje hoja na aitolee maelezo katika aya moja.

3. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali hii

Ukicheza ujanani utalipa uzeeni.

MATUMIZI

Hutumiwa kuwahimiza watu wajitahidi kujitengenezea maisha yao ya kesho/mustakabali wao wakiwa wangali na uwezo wa kufanya hivyo.

TANBIHI

a) Mtahiniwa sharti aandike kisa kitakachodhihirisha maana ya methali

b) Kichwa kionyeshe pande mbili za methali:

-kucheza ujanani

-kulipa uzeeni

c)Mtahiniwa atakayerejelea upande mmoja atakuwa amepungukiwa kimaudhui. Insha yake isizidi alama **10**

d)Atakayeandika kisa kisichohusiana na methali hii atakuwa amepotoka kimaudhui. Atuzwe alama **03**.

e) Atakayejitungia swali na kulijibu atuzwe **BK 01**

f) Dhana ya kulipa uzeeni ijitokeze hata kama ni kwa aya chache/sentensi chache.

4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo.

...sasa ninaelewa maneno yake kuhusu kufanya maamuzi ya hekima au busara.Sasa nimepata baraka za wazazi na ridhaa ya kuishi pamoja.

MAJIBU

- Hii ni insha ya mdokezo

-Mtahiniwa ajihusishe na kisa (nafsi ya kwanza)

-mtahiniwa amhusishe pia aliyempa wosia(nafsi ya tatu)

-Ruwaza ya kisa idhihirike kwamba mhusika alikuwa amepotoka na kuvuruga uhusiano na wazazi wake **LAKINI** akapata mawaidha/mwelekeo/wosia kutoka kwa mhusika mwingine na uhusiano mwema ukarejeshwa baina yake na wazazi wake.

Baadhi ya visa ni;

- a) Mhusika anayetoroka nyumbani kwa kukosana na wazazi ,apewe ushauri kisha aamue kurudi kuomba msamaha na kuendeleza maisha pamoja na wazazi wake.
- b) Mhusika anayetamauka kimasomo kwa sababu fulani .Jambo hili livuruge uhusiano na wazazi wake ,apewe ushauri na mwalimu au mwanafunzi mwenzake, asome afaulu na kufurahisha wazazi wake.

visit www.freeksepastpapers.com to download free resources